Namba (01)

أَقْوَالُ عُلَمَاءِ الشِّيْعَةِ الْإِمَامِيَّةِ

فِيْ حَقِيْقَةِ مَقْتَلِ الْحُسَيْنِ -رَضِيَ اللهُ عَنْهُ-

KAULI ZA MAULAMAA WA SHIA IMAAMIYYAH

KUHUSU UKWELI WA KIFO CHA HUSEIN -ALLAAH AMRIDHIE-

Amesema Ibn Taymiyyah -Allaah amrehemu-:

"وَأَمَّا مَنْ قَتَلَ الْحُسَيْنَ أَوْ أَعَانَ عَلَى قَتْلِهِ أَوْ رَضِيَ بِذَلِكَ فَعَلَيْهِ لَعْنَةُ اللَّهِ وَالْمَلَائِكَةِ وَالنَّاسِ أَجْمَعِينَ"

"Ama yule aliyemuuwa Hussein, au alitoa msaada juu ya kuuwawa kwake, au aliridhia jambo hilo, ishuke juu yake laana ya Allaah, Malaika na laana ya watu wote". [Majmuu'l fataawa] (Jz. 4, Uk. 487).

Mwandishi:

Abu Halima Arafat Bin Mahmoud

Kauli ya Kwanza: Amesema Murtadhwa Mutwahariy[1] katika kitabu chake [Al Malhamatul Husayniyyah] (Jz. 3, Uk. 94):

"فَنَحْنُ سَبَقَ لَنَا وَأَثْبَتْنَا أَنَّ هَذِهِ القِصَّةَ مُهِمَّةٌ مِنْ هَذِهِ النَّاحِيَةِ، وَقُلْنَا أَيْضًا أَنَّ مَقْتَلَ الْحُسَيْنِ (ع) عَلَى يَدِ الْمُسْلِمِيْنَ بَلْ عَلَى يَدِ الشِّيْعَةِ"

"Hapo awali tumethibitisha kwamba kisa hiki ni muhimu sana katika suala hili, na pia tulisema kwamba kuuawa kwa Hussein رضي الله عنه kulikuwa mikononi mwa Waislamu, bali mikononi mwa Shia (wafuasi wake)".

Pia amesema tena katika [Jz. 1, Uk. 129]:

"وَلَا رَيْبَ فِيْ أَنَّ أَهْلَ الْكُوْفَةَ كَانُواْ مِنْ شِيْعَةِ عَلِيِّ بْنِ أَبِيْ طَالِبِ (ع) وَأَنَّ الَّذِيْنَ قَتَلُواْ الْإِمَامَ الْحُسَيْنَ (ع) هُمْ شِيْعَتُهُ»"

"Hapana shaka kwamba watu wa Mji wa Kufa walikuwa ni katika wafuasi wa Ally Bin Twalib رضي الله عنه na kwamba waliomuuwa Imam[2] Hussein رضي الله عنه ni Shia (wafuasi wake), kwa saabu hiyo wameandika wanahistoria kuhusu watu wa Kufa wanasema: [Mioyo yao ipo pamoja naye 'Hussein' na panga zao zipo dhidi yake]".

Kauli ya Pili: Amesema Sheikh Kaadhim Hamad Al Ahsaaiy katika kitabu chake: [Min Majaalis 'Aashuraa] (Uk. 89), katika Majlis ya 15:

"إِنَّ الْجَيْشَ الَّذِي خَرَجَ لِحَرْبِ الْإِمَامِ الْحُسَيْنِ (ع) كَانَ ثَلاَثَ مِائَةِ ألفٍ، كُلَّهُمْ مِنْ أَهْلِ الْكُوْفَةِ، لَيْسَ فِيْهِمْ شَامِيٌّ، وَلَا حِجَازِيٌّ، وَلَا هِنْدِيٌّ، وَلَا بَاكِسْتَانِيٌّ، وَلَا سُوْدَانِيٌّ، وَلَا مَصْرِيٌّ، وَلَا إِفْرِيْقِيٌّ، بَلْ كُلُّهُمْ مِنْ أَهْلِ الْكُوْفَةِ"

"Hakika askari waliotoka kwenda kupigana na Imam Hussein رضي الله عنه walikuwa laki tatu, wote wanatoka Mji wa Kufa, hakuna miongoni mwao mtu wa Sham, Hijaz, India, Pakistan, Sudan, Misr, wala Afrika, watu wote ni kutoka mji wa Kufa".

---

[1]- Mwanachuoni wa Kishia wa karne ya kumi na nne, amezaliwa mwaka 1919m na kufariki 1979m, ni miongoni mwa wanafunzi wa Twabatwaaiy na Khomein.

[2]- Mashia humuita Hussein Imam lakini ukweli ni kwamba yeye hakuwahi kuwa Khalifa رضي الله عنه

Kauli ya Tatu: Na amenukuu Sayyid Husein An Naraaqi An Najafiy katika kitabu chake: [Taarikhul Kuufah] (Uk. 113) kutoka kwa Al Qazwiiniy amesema:

"وَمِمَّا نُقِمَ عَلَى أَهْلِ الْكُوْفَةِ، أَنَّهُمْ طَعَنُوا الْحَسَنَ بْنَ عَلِيٍّ (ع) وَقَتَلُوا الْحُسَيْنَ (ع) بَعْدَ أَنِ اسْتَدْعُوْهُ"

"Miongoni mwa mambo ambayo hulaumiwa watu wa Kufa ni kwamba wao wamemchoma mkuki Hassan Bin Ally رضي الله عنهما na wamemuua Hussein -alayhis salaam- baada ya kuwa wamemuita".

Kauli ya Nne: Amenukuu sheikh Muhsin Al Amin katika kitabu chake: [A'ayaanu Sshii'ah] (Jz. 1, Uk. 26), kutoka kwenye kitabu kiitwacho: [Ad Darajaatu Rrafii'ah], cha Sayyid Ally Khan amesema:

"ثُمَّ بَايَعَ الْحُسَيْنَ مِنْ أَهْلِ الْعِرَاقِ عِشْرُوْنَ أَلْفًا غَدَرُوا بِهِ، وَخَرَجُوا عَلَيْهِ، وَبَيْعَتُهُ فِيْ أَعْنَاقِهِمْ، فَقَتَلُوْهُ"

"Kisha watu Elfu ishirini wa Iraq walimpa Bai'a (kiapo cha utiifu) Hussein kisha wakamfanyia khiyana, na wakatoka dhidi yake (ili wamuue), hali ya kuwa Bai'a yao ipo juu ya shingo zao".

Kauli ya Tano: Kauli ya mmoja katika Ahlul Bayt kama alivyonukuu sheikh wao Ahmad Bin Ally At Twabarsiy, katika kitabu: [Al Ihtijaaj] (Jz. 2, Uk. 27), wakati Zainab Bint Ally Bin Abi Twalib ndugu yake Husein رضي الله عنه akiwalaumu watu wa Kufa kwa kumuua kaka yake Husein رضي الله عنه

"أَتَبْكُوْنَ عَلَى أَخِيْ؟! أَجَلْ واللهِ، فَابْكُوا فَإِنَّكُمْ أَحْرَى بِالْبُكَاءِ فَابْكُوا كَثِيْرًا، وَاضْحَكُوا قَلِيْلاً"

"Hivi leo mnamlilia ndugu yangu?! Wallaahi ni vizuri, basi lieni sana kwa sababu nyinyi mnastahiki zaidi kulia, na mcheke kidogo tu".

Wallaahul muwaffiq.

Abu Halima Arafat Bin Mahmoud
Jumanne ya 10/Muharram/1446h – 16/07/2024m.
Simu: 0715263253
Tanga Tanzania.